

NEEMA YA KIWANDA CHA SUKARI YAJA KILOSA

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe John Pombe Magufuli atangaza neema ya kiwanda cha sukari katika kata ya Mbigiri wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, lengo ikiwa ni kutimiza kile alichohidi kwa wananchi kuona katika awamu ya tano tunakuwa Tanzania ya uchumi wa viwanda.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya Kilosa Mhe Idd Mgoi katika kikao cha mwisho cha kufunga mwaka cha baraza la madiwani kilichohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa mkoa wa Morogoro katika ukumbi wa Kilosa club.

Mheshimiwa Rais ameamua kuachia lulu ya uwepo wa kiwanda cha sukari wilayani Kilosa , ambapo kiwanda hicho kisaidia kujikwamua kiuchumi na kuwa na uchumi wa kati ambao utaufadisha wilaya, mkoa , mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, hivyo tuitumie vyema nafasi hii kwa manufaa ya wanakilosa wote na kuachana na dhana ya kutumia ardhi kwa ubinafsi. Aliongeza Mgoi.

Mh.Mgoi amewataka watendaji wa Halmshauri kuweka mpango mzuri wa matumizi bora ya ardhi katika kata za Msowero na Mvumi ambazo ndizo zina mashamba tisa yaliyofutwa baaada ya kuhodhiwa bila kuendelezwa, ambapo ametaka maeneo yatengwe kwa ajili ya matumizi ya wananchi, uwekezaji na matumizi mengine.

Sambamba na hayo amewataka waheshimiwa madiwani kusimamia vizuri mipango hiyo ya matumizi ambapo utekelezaji wake utaleta tija na matokeo mazuri na kuifanya Kilosa kuwa wilaya ya mfano wa kuigwa na wilaya nyingine ndani na nje ya mkoa wa Morogoro.